KUSIMAMISHA KANISA

Kusimamisha Kanisa: Muhtasari

Maelezo Mafupi -

DARASA LA #1:

I. Utangulizi wa Kosi.
II. Kusimamisha Kanisa na Biblia.
III. Sababu Ambazo Kusimamisha Kanisa Huonyesha kuanguka.
IV. Andiko la Msingi na Mawazo ya Kusimamisha Kanisa.
V. Hatua Sita za Kusimamisha Kanisa.

DARASA LA #2:

VI. Timu za mitume na Mafunzo ya "Nenda Peana/Ondoka."

DARASA LA #3:

VII. Mazoezi 12 ya Kusimamisha Kanisa.

DARASA #4:

VII. Mazoezi 12 ya Kusimamisha Kanisa (yanaendelea.).

DARASA #5:

VII. Mazoezi 12 ya Kusimamisha Kanisa (yanaendelea.).

Kusimamisha Kanisa: Mtihani

Maswali Yanayoweza Kupewa Pointi 20

1) Eleza jinsi kamuni ya kuzidisha ilianza katika Mwanzo na jinsi inahusiana na kusimamisha Kanisa (kwiasa. 208-210).
2) Orodhesha na ufafanue hatua sita za Yoder za kusimamisha Kanisa (Kwiasa. 212-214).
3) Kundi la mitume ni gani na mafunzo ya Nenda/Peana/Ondoka ni gani? kwa nini mawazo yote mawili ni ya muhimu sana katika kusimamisha Kanisa (kwiasa. 216-221)?
4) Fafanua kusimamisha Kanisa kama mazoezi ya kufanya ufahamiano na watu (uk. 227).
5) Fafanua kanuni nyingine za huduma zinazotumiwa katika kusimamisha Kanisa mazoezi ya kubatiza na kupokea washirika katika Kanisa jipya (kwiasa. 235,236).
6) Kundi la kusimamisha Kanisa linawezaje kutayarisha waamini wapya? (kwiasa. 242,243).

Maswali Yanayoweza Kupewa Pointi 10

1) Tumia 1 Kor 3:10-15 kuonyesha yale, Mungu anahusika nayo sana katika kusimamisha Kanisa (uk. 210).
2) Orodhesha sababu tatu ambazo zaonyesha kwanini miradi ya kusimamisha Kanisa haifaulu (uk. 211).
3) Mith 24:10 inatumiaje kusimamisha Kanisa (uk. 212)?
4) Orodhesha njia tatukuwavutia watu wapya kanisani (uk. 215).
5) Taja huduma tano zinazo patikana katika waefeso 4:11 na malengo yanayoandamana nao katika kustawisha kanisa (uk. 216).
6) Orodhesha sababu mbili kwanini wamishoanari hawaondoki (uk. 219).
7) Kwanini twaweza kusema kwamba sehemu ya "kwondoka" ya kusimamisha kanisa ndiyo ya muhimu sana? (uk. 220)
8) Kwanini kundi la mitume lazima liondoke marakama iweza kanavyo? Toa sababu mbili (uk. 220).
9) Nini "kutengwa na Mungu”? (p. 230)
10) Orodhesha mambo matatu ya nsingi kufundisa waamini wapya (uk. 232).
11) Orodhesha amri tatu muhimu ambazo lazima zifunzwe katika mkutano wa kwanza wa Kanisa (uk. 237).
12) Orodhesha maswali matatu ambayo ungeyaffikiria wakati unakata kauli juu ya matindo unaofaa wa kuabudu kwa kanisa jipya lililosimamishwa (uk. 239).

KUSIMAMISHA KANISA

Maelezo Mafupi -

I. Utangulizi wa Kosi.

A. Umuhimu wa kusimamisha Kanisa.

1. Lengo la winjilisti ni kuongeza kanisani. Malengo yetu lazima yalenge juu ya kumfanya bibi arusi aonekane anastawi (Waefeso 5:27). Kanisa ni bibi arusi.

2. Kanisa ni sehemu ya msingi ya Ukristo. Ni mwili wa mwanzilizi na kiongozi.

   a. Kwa hivyo, kusimamisha kanisa ni kusimamisha Ukristo.

   b. Kusimamisha Kanisa ni kusimamisha neno la Kristo.

B. Kusudia Kosi Hii.

1. Katika kosi hii tunatumaini kupata misingi ya kufahamu kusimamisha kanisa.

2. Kosi hii inampatia mwanafunzi maono, mawazo, na vifaa kwa ajili ya kusimamisaha Kanisa.

3. Tutajifunza aina kadha za mambo ya kusimamisha kanisa katika sehemu ya kwanza ya kosi.

4. Katika sehemu ya pili ya kosi tutapata kutoka kwa aliyozola George Patterson ambaye alisimamisha mamia ya makanisa katika Honduras.

   a. Kosi hii itatoa muhtasari wa maelezo yanayopatikana katika kitabu chake kiitwacho "Uongozi wa kusimamisha kanisa."[1]

   b. Katika masomo hayo tutafikiria yale Petterson ameyaita mazoezi 12 ya kusimamisha kanisa.

5. Natuanze kwa kufikiria mafunzo mengine ambayo msingi wake ni juu ya mazoela ya msimamishaji mwingine wa Kanisa aliyepata ushindi, Larry Tomczak.[2]

KUSIMAMISHA KANISA

Maelezo Mafupi –

II. Kusimamisha Kanisa na Biblia.

A. Biblia inasema nini juu ya kusimamisha Makanisa?

1. Kama tunataka kuwa na matokeo ya Agano Jipya, basi inatupasa kurudi kwa mpango wa agano Jipya wa kusimamisha Kanisa (Matendo 2:41).

2. Kuna njia nyingi za uinjilisti. Hata hivyo, katika Agano Jipya njia ya kusimamisha Kanisa ilitumiwa mara nyingi kwa uinjilisti.

3. Kutimiza Mwito Mkuu (ambao maana yake ni kufanya wanafunzi sio tu kupata watu "wakate kauli"kuwa Wakristo) inatupasa kusimamisha makanisa.

4. Lazima tulenge juu ya kuzidisha lazima pawe na kuzidisha kwa kiroho.

   a. Kuleta matunda mazuri ya juu kutatokea mara katika kuleta matunda mazuri makubwat.

   b. Masomo ya kuzidisha hutafuta kueneza injili na kufunza mitume watu kundi dogo ili kuwambukiza sehemu kubwa (tazama Matendo 19:1-10).

5. Kannuni ya kuzidisha ilianza katika Mawanzo na Adamu na Hawa.

   a. Waliamriwa wazidishe (Mwa 1:28). Hawakuambiwa "waongeze”.

   b. Hawakujaza ulimwengu wote wao wenyewe walizaa wenyewe.

   c. Watoto wao basi walizaona wao wenyewe.

KUSIMAMISHA KANISA

Maelezo Mafupi –

Mahali Pa Majadiliano

Jifunze na ujadili mchoro ufuatao unaohusiana na kanuni ya kuzidisha kama ulivyoonyeshwa na Adamu na Haawa.

Haikutendeka hivi. Huku ni kuongeza



Ilitendeka hivi. Huku ni kuzidisha



6. Kutumia kanuni hii ni kwa lazima katika kusimanisha makanisa. Hatutaki kunda kuitegemea. Tunataka kuzidisha (kuzaa) wale watakaofanya jambo hilo hilo (kuzaa wengine) (tazama 2 Tim 2:2).

7. Tunahitaji kusimamisha makanisa ya mitaa yanapumia uzima wa kanisa la Agano Jipya.

   a. Ujumbe lazima uwe wenye nguvu na ulionyoka wenye himizo WAZI kutubu na kuamini (Matendo 2:36-39).

   b. Fikirira (maono) ya kusimamisha kanisa.

      1) Ulimwengu si kutatanisha tu. lnaeleweka kwamba maisha ya ulimwengu yako kinyume kwa kushambulia maisha ya Mkristo (Matendo 2:40).

      2) Kwa hivyo, ijapokuwa hatuwezi kutenganishewa na ulimwengu, lazima tujitenge na ulimwengu.

   c. Njia ya mpango.

      1) Kila Mkristo inampasa kuwa sehemu ya lazima ya kanisa la mtaa. kila mshirika wa mwili lazima afanye kazi katika mwili.

      2) Ukristo si mikutano tu. Ni maisha yanayoshirikianwa ndani ya umoja wa imani.

      3) Mundo na mpango wa Kanisa msingi wake si juu ya mikutano na mpango. Msingi wake ni uhusiano.

      4) Mungu hahusiki na vile tunaweza kujenga kanisa haraka. Anahusika na nzuri wa kazi (1 Kor 3:10-15).

8. Kanisa linasi shwa na kundi la mitume (waefeso 4:11; 1 Kor 12:28). Paulo alifanya kazi na kundi (Matendo 13:2, 5, 13; Matendo 20:34; Matendo 22:6). Tuasema zaidi juu ya makundi ya mitume baadaye kosini

Mahali Pa Majadilino

Tumia mchoro ufuatao kufanya muhtasaru wa maoni yaliyo sawa ya Kanisa.

Kichwa chake	Siyo	Ndiyo
Ukristo	Mkutano	Maisha ya ushirika
Mundo wa kanisa	Msingi wake ni juu ya mikutano na mipango	Msingi wake ni uhusiano wa kweli
Yanayohusika na Mungu	Jinsi tunavyojenga Kanisa haraka	Uzuri wa kazi
Kanisa	Shughuli au shirika	Mwili

III. Sababu kadha kwanini kusimanisha kanisa kama mradi hukosa kufaulu.

A. Kulikosekana nini?

1. Kukosa mwongozo wazi na hekima kutoka kwa mungu katika hatua za kupanga.
2. Kukosa vipawa vizuuri katika huduma katika kundi.
3. Kukosa maombi (hatayaliyo ya lazima katika kazi ya mwanzo).
4. Kukosa pesa (watu na pesa).
5. Kukosa tabia na utu uzima katika viongozi.
6. Kukosa mafunzo.
7. Kukosa kuwa na lengo halisi na utawala (maono na mpango).
8. Kukosa umoja katika kundi.
9. Kukosa kufahamu lengo la utamaduni.
10. Kukosa mapenzi ya kupokea utamaduni mpya (yaliyomo, ambayo niya lazima kureke bisha katika mundo unaoukubali ujumbe wa Mungu kuwako baina ya ntamaduni na wakati).

Maelezo Mafupi –

Mahali Pa Majadiliano

Jadili ujuzi wako wa mazoea katika kwezo wa kusimamisha makanisa an yale ambayo umeyaona yamesimamishawa Je, kuna moja ya shida zilizoorodheshwa hapo juu ambayo ilikuwa shida katika uwezo wa kusimamisha makanisa?

IV. Andiko la msingi na Mawazo kwa kusimamisha Makanisa.

A. Maandiko kwa kusimamisah makanisa.

1. Mith 24:10.
2. Zek 4:10.
3. Wagalatia 6:9.

B. Mawazo ya kukariri na kujadili.

1. Omba kama kwamba vitu vyote vinategemea Mungu fanya kazi kana kwamba vitu vyote vinategemea kundi.
2. Rudia na ukumbuke kila maria yale Mungu amekwisha kujafanya. Hili litaku saidia kuwa na imani kwa ushindi wakati ujao.

V. Sehemu Sita za kusimamisaha kanisa (na Glen Yoder)[2].

A. Sehemu #1: Wazo.

1. Huu ni mwanzo. Ni sehemu ya kupanda makanisa inayotendeka kabla ya wewe kuondoka kwenda mahali panapolengwa.
2. Katika sehemu hii maono na mpango zinazaliwa na kwendelezwa.
3. Kundi linatumia wakati mwingi pamoja na kwanza kunda uhusiano wenye nguvu.

B. Sehemu #2: Kabla - Ya - Kuzaliwa.

1. Sehemu hii hutukia kabla katusa halijakuwa mahali pa kuabudiwa na "watu wote".

2. Kundi la kusimamisha makanisa huwaendea jamii. Hufanya uinjilishti wa mtu binafsi na watu wote.

3. Wanafunzi wa kwanza wanaundwa katika makundi madogo. Panaweza kuwa na makundi madogokadha yanayokutana katika nyumba kadha.

4. Huduma za msingi zinaundwa. Dhehebu la msingi linafunzwa.

C. Sehemu #3: Kuzaliwa.

1. Kanisa linaanza kuwa mahali pa kuabudia pa watu wote panapowe zekana. Katika utamaduni unaokataza, hekima na ujasiri lazima zifikiriwe.

2. Mafunzo na njia ya kuabudu iendeshwe.

3. Watu wote wanalikwa kuhudhuria mikutano ya umati jumapili.

D. Sehemu #4: Maisha ya Mwanzoni.

1. Waongofu wanaojitolea kwa nguvu kwa Yesu kuanza kuchukua madaraka zaidi kwa kukata kauli na mambo yanayofanywa kanisani.

2. Kupeanwa kwa mamlaka kunaanza. Kuzaliwa kwa viongozi na vipawa huanza.

E. Sehemu #5: Kukua mapaka kuwa mtu mzima.

1. Fikiria la kuwa na msimamo na utu nzima kunaendelezwa.

2. Lengo ni juu ya mafunzo ya wongozi.

3. Kuna wazi wa maendeleo ya kuzidisha wongozi na huduma.

4. Kuna hakika ya mpango kuongezeka katika mwili wa waaminio.

F. Sehemu #6: Kuzaa.

1. Kanisa linaanza kuzaa - kusimamisha makanisa wengine na kuhudumia watu wanaowatembe lea.

2. Uinjilisti na umishonari zinaanza kutiliwa mkazo.

3. Kanisa linatuma wamishonari kuanza makanisa mapya.

KUSIMAMISHA KANISA

Maelezo Mafupi –

Mahali Pa Majadiliano

Jifunze na ujadili mchoro ufuatao (na Glen Yoder) wa sehemu sita za kusimamisha makanisa

- Sehemu sita za kusimamisha makanisa ni gani?
- Kufanywe nini katika kila sehemu ili kusimamisha kanisa?
- Ni aina gani ya mafunzo yanayolingana na kila sehemu?
- Jaribu kueleza na upeane mifano ya mazoezi ya kila sehemu.



KUSIMAMISHA KANISA

Maelezo Mafupi -

Ifuatayo ni orodha ya mipango kuvutia kuongezeka kwa watu kanisani. Orodha hii inawakilisha tu mawazo na si orodha kamili ya uwezekano. Unda orodha yako mwenyewe ya njia zenye misingi juu ya kweli ya hali.

1. Omba Bwana wa mavuno (Mt 9:38).

2. Fanya mazoezi ya ukarimu. Alika watu nyumbani mwako. Uwe na pikiniki ya jirani.

3. Peana mafunzo ya nyumbani ya Biblia juu ya mambo maabumu ya kupendeza ambayo yangekuwa yanalenga watu wa kundi hilo (ndoa, kulea watoto, ushindi katika fedha, nk.).

4. Panga michezo maalumu ya watoto.

5. Matangazo (radio, television, kariatasi za matangazo, vikaratasi vya matangazo, n.k).

6. Peane mialiko ya mtu binafsi. shuhudia wale unaokutana nao katika hali za kawaida.

7. Fanya uinjilisti wa mtu binafsi. Shuhudia wale unaokutana nao katika hali za kawaida.

8. Fanya uinjilisti wa nyumba kwa nyumba.

9. Fanya uinjilisti wa barabarani (uwanjani, pembe ni mwa njia, lemani).

10. Fuatilia. Tuma barua na uwatembeleewale wanaotembea kani sani kwa mara ya kwanza.

Maelezo Mafupi –

VI. Makundi ya mitume na mafunzo ya "Nenda/Peana/Ondoka"”.

A. Makundi ya Mitume.

1. Kundi la Mitume linafanywa katika msingi wa huduma tano zinazopatikana katika Waefeso 4:11:

   a. Mitume - wale wanaotumwa kupanga kazi mpya (hawa si wale mitume 12 wa mwanzo katika Agano Jipya).

   b. Manabii - wale ambao ujumbe wao huwaita watu wa Mungu kundi katikati mwa kanuni wanazozitangaza.

   c. Wainjilisti - Walio na mwito maalumu wa kujenga kanisa.

   d. Wachungaji - walio na uwezo maalumu wa kulisha wanafunzi kwa njia zote za maisha ya ukristo na Kanisa.

   e. Walimu - walio na uwezo wa kutia nguvu waamini kwa hekima ya mazoea kwa maisha ya Mkristo na huduma.

2. Kila moja ya huduma hizi lazima ifanye sehemu yake kuimarisha kanisa.

   a. Mitume na manabii hulenga kusimamisha musingi na kupeana mwelekeo.

   b. Mwinjilisti hulenga unjilisti.

   c. Wachungaji hulenga huduma ya uchungaji.

   d. Walimu hulenga walimu.

3. Hii si kusema kwamba walimu hawawezi kufundisha, n.k Tunazungumza hapa kwa njia ya kutia makazo na lengo tu.

4. Aina kadha za kukua kwa kanisa kutatokea katika lengo juu ya huduma kadha.

KUSIMAMISHA KANISA

Mahali Pa Majadiliano

Maelezo Mafupi -

Fikiria na ujadili mchezo ufuatao unaohusiana na aina tofauti za kukua kuwa wa kutumika kanisani.

Aina za kukua	Wataalamu
Kukua kwa kwanza	Mtume, Nabii Mwinjilisti
Kukua kwa ndani (uzuri)	Mchungaji Mwalimu
Kueneza kukua (wingi)	Mwinjilisti
Kukua kwa kupanika (kuanza makanisa dada mpya	Mwinijilist, Mwalimu, Mtume
Kukua kwa daraja (umishonari)	Mtume, Nabii
Kukua kwa maono (kwa kawaida)	Nabi

5. Baada ya kusimamisha kanisa, kila huduma peke yake lazima ianze kuambatana na mafunzo na kuzaa.

    a. Wainjilisti wafunze wengine kuwa wainjilisti.

    b. Wachungaji wafunze wengine kuwa wa chungaji, n.k.

        1) Wazo ni kuzalisha kipawa chako.

        2) Lengo ni kuyitoa kazini (ili wengine waweze kufanya huduma hiyo).

6. Baada ya kuwa na fikira kwamba vipawa vimezaliwa kundi linaondoka ili kufanya jambo hilo hilo katika mtaa mwingine ambao haujafikiwa.

7. Kanisa liliosimamishwa linafunzwa kutuma "kundi lao la Mitume" katika mtaa ambao haujafiriwa.

    a. Mwenendo huo huo wa kuzalisha vipawa lazima utendeke ndani ya Kanisa.

    b. Matokeo lazima yawe kwamba "makundi kadha ya mitume" yaweze kutumwa nje.

    c. Huu ni mwanzo wa ASILI wa kuzidisha makanisa.

Maelezo Mafupi –

Mahali Pa Majadiliano

Makundi haya ya Mitume yanatofautianaje na makundi ya kusimamisha makanisa ya venyeji?

B. Mafunzo ya "Nenda/Peana/Ondoka".

1. Kundi la Mitume lazima liwe na mafunzo ya huduma. Twaweza kuita mafunzo haya "Nenda/Peana/Ondoka".

   a. Nenda (tazama Mt 28:19; Mwanzo 12:1).

      1) Wamishonari lazima "WAENDE kutii amri ya Kristo.

      2) Wamishonari lazima waondoke kutoka nyumba ni mwao binafsi na "kwenda" kwa mataifa ya ulimwengu.

   b. Peana (tazama Mt 28:19, 20; Mwa 12:2, 3; Mt 10:8; 2 Tim 2:2).

      1) Wamishonari lazima wapeane bure kile walichopata bure.

      2) Hadithi kwa ya umishonari iko katika Yn 3:16. Mungu ALITOA. Yesu AKAENDA

   c. Ondoka (tazama Yn 16:7; 2 Tim 2:2; Matendo 14:23; Wafilipi 1:6: Matendo 20:32; Matendo 20:29, 30).

      1) Wamishonari lazima waondoke pia. Yesu ALIONDOKA ili Roho mtakatifu aweze kumaliza kazi. Paulo ALIONDOKA kwa sababu ya kusudi hilo hilo. Roho mtakatifu alifanye kanisa kukomaa. KUONDOKA ni sehemu ya lazima wazo la kuzaana (tazama 2 Tim 2:2).

      2) Kuna uwezekano wa kupoteza ulioko (tazama Matendo 20:29, 30). Ndiyo sababu tuna imani kuachilia ni kufanya likue. ONDOKA ni sehemu ya lazima ya umishonari

2. "ONDOKA" mara nyingi ndiyo sehemu iliyo ngumu zaidi ya mafunzo yanayofikirwa. Pia ndiyo inayoharibiwa zaidi. Wamishonaari wengi HAWAONDOKI mahali wapokwenda Kwanini?

   a. Hili linatendeka wakati wamishonari wanataka kujaribu kujenga ufalme wao wenyewe.

   b. Hili linatendeka wakati wamishonari wana mawazo ya chini (kuhukumu) juu ya uwezo wa wenyeyi. Wanajisikia kwamba hawawezi kufanya kazi sawasawa.

   c. Hili linatendeka wakati wamishonari wana mawazo ya juu sana (kiburi) juu ya uwezo wao wenyewe. Hakuna mwingine anayeweza kuifanya vizuri kama wao wanavyoweza.

   d. Hili hutendeka wakati wamishonari wana imani haba. Wanachagua kuweka imani nyingi katika wao wenyewe na kwa hivyo wanaimarisha mwenendo wa kusimamia wawe na fikira ya usalama.

   e. Hili linafanyika wakati wamishonari ni wavivu. Wanajisikia kubuwudika katika maisha ya umishonari.

   f. Hili hutendeka wakati wamishonaari hawaweki lengo katika fikira zao kuelekea yale umishonari unafanya (Mt 24:14; Warumi 15:20, 21).

   g. Hili hutendeka wakati wamishonari wanajaribu kujenga mashirika na miradi badala ya ufalme wa Mungu hivyo, wamekuwa wanahusika na kutumia wakati mwingi kwa miradi ambayo mara nyingi haina faida ya kudumu

   h. Hili hutendeka wakati wamishonari wanafikiria kwamba "kwenda polepole" maana yake "tunazalisha tunda linalofaa zaidi" kuna bei ya juu inayotiwa katika "sadaka" ya kuwa mahali pamoja kwa miaka 20. Paulo hangekubali. Angesema kwamba "nguvu" maana yake ni nzuri (tazama Matendo 20:31).

   i. Hili hutendeka wakati wamishonari hawa fahamu kanuni za kukua kwa asili. Makanisa hukua kiasili wakati yamepewa uhuru kukua kiasili. Hayakui kiasili wakati yanapoamishwa na "kulishwa kwa kijiko" Makanisa ambayo yanategemea wamishonari si makanisa yenye afya

   j. Hili linatendeka wakati wamishonari wanzungumza juu kufundisha watu jinsi ya kuvua samaki ili waweze kujivulia samaki wenyewe (badala ya kuwavulia samaki). kwa bahati mbaya, wengi hawatii katika mazoezi kanuni hiyo.

Mahali Pa Majadiliano

Ujuzi wako wa Nenda/Peana/Ondoka umekuwaje ambazo ni kanuni za umishonari? Jadili na ukubali mawazo.

3. Sehemu ya KUONDOKA ya umishonari ndiyo mara nyingi iliyo ngumu iliyo ngumu zaidi kwa sababu wamishonari lazima watoe waliyofa kwa nguvu kuanzisha. Kwa fikiria hizi, sehemu ya KUONDOKA kwa kweli ni ya pili ya sehemu ya PEANA. wamishonari lazima WAPEANE ili WATOE.

4. Sehemu ya**ONDOKA** ya umishonari mara nyingi ndiyo ya muhimu kwa sababu ndiyo sehemu inayokubali kanisa changa kukua kiasili. Nenda na**PEANA** hukubali kanisa kuzaliwa kiasili. **ONDOKA** hukubali kanisa kukua kiasili.

5. Kumbuka: Paulo na makundi yake WALIKWENDA ili KUONDOKA. HAWAKUENDA ili wakae. Walizidisha ufalme wa Mungu kwa kuzidisha huduma. Walianzisha huduma. Kisha haraka iwezekanavyo, walipeana huduma kwa wale walioishi hapo wale kwa kweli wangeweza kuifanya vizuri zaidi kwa sababu wangeifanya kiasili zaidi. Waliishi hapo. Walikuwa viongozi wa asili na waliwajua watu wao na utamaduni wao.

   a. Kundi la Mitume lazima liondoke haraka iwezekanavyo (bila kuondoka haraka kabla misingi haijawekwa) kwa sababu mbili:

      1) Kufanya kanisa kukua kiasilikatika wongozi wenyeji kanisa lazima lijitawale.

      2) Kuendelea na kazi ya mitume. Kundi lazima liondoke ili kusimamisha makanisa katika sehemu ambazo hazijafikiriwa.

   b. Paulo aliweza kuwa na mafunzo haya kwa sababu alimwamini Roho Mtakatifu. Aliweka imani yake kwa Mungu kukamilisha kazi (Wafilipi 1:6).

KUSIMAMISHA KANISA

Maelezo Mafupi -

Mahali Pa Majadiliano

Mchoro ufuatao unasaidia kueleza huduma ya "makundi ya mitume" na mafunzo ya huduma yaitwayo "Nenda/Peana/Ondoka" sababu kubwa ni KUZAANA. Jadilli mawazo haya na ujibu maswali yo yote



VII. Mambo 12 ya kusimamisha Makanisa.

Maneno Ya Mwandishi:

Mambo yafuatayo 12 yametokana naUongozi wa kusimamisha Makanisa na , George Patterson.[1] lmetumiwa kwa kuhusiwa.

A. Jambo #1: Tafuta Uongozi Wa Bwana.

1. Kuanza.

   a. Maombi ndilo jambo la muhimu sana katika kusimamisha makanisa (tazama Mith 3:5, 6).

      1) Yesu aliomba kabla ya kwenda katika mahali papya (Mk 1:35-39).

      2) Petro alikuwa akiomba wakati Mungu alimwonyesha mpango wake (Matendo10:9).

   b. Katika jambo hili tutafanya haya:

      1) Omba ili kukata kauli ni wapi patasi mamishwa kanisa jipya.

      2) Fanya mpango wa kuzidisha makanisa kiasili.

2. Nisimamishe kanisa wapi?

   a. Omba na ulize Mungu maono na mzigo wa mahali maalimu

   b. Kutana na viongozi wengine ambao wangependelea kusimamisha kanisa. Mwulize Mungu aunde kikundi.

      1) Ombeni pamoja mara kwa mara.

      2) Kubali mashawu ya wengine.

      3) Tafuteni umoja katika kundi. Mungu aweza kubariki umoja. (Ps 133:1-3).

      4) lkiwezakana, tembea mahali hapo panapofikiriwa.

Maelezo Mafupi

c. Maswali ya kufikiria.

1) Mtaa huo uko mbali kiasi gani?

2) Umekwisha kuanza kuhubiriwa?

3) Una wakristo wangapi?

4) Watu wanaoishi hapo wanapokeaje injili?

5) Makanisa ya hapo yanashuhudia kwa uwezo na kuhubiri?

6) Kuna rafiki au jamaa wa wakristo wengine wanaoshi hapo? Watakwenda nasi kutembea?

7) Je, pana watu wapya wanaohamia mahali hapo?

8) Watu hufanya kazi za aina gani?

9) Watu wana shida za namna gain?

10) Hali yao ya uchumi ikoje?

11) Watu hawa hufanya nini kwa kujifurahisha?

12) Je, kuna watu makundi tofauti wanaoishi katika mahali hapo hapo?

3. Nawezaje kupanga juu ya kuzidisha makanisa?

a. Ehora ramani rahisi ya mahali ulipopachagua.

b. Kata kauli juu ya mahali pa muhimu kusimamisha kanisa, la kwanza.

c. Kata kauli juu ya mahali pengine kadha ambapo makanisa yange simamishwa.

d. Fikiria vile kanisa la kwanza lingaliweza kuanza makanisa kadha.

1) Tia katika masomo ya mafunzo ya wazee wenyeji wawe viongozi wa kuhudumia.

2) Panga kuwafunza viongozi wenyeji ambao watakwenda kusimamisha makanisa sehemu nyingine.

KUSIMAMISHA KANISA

Maelezo Mafupi –

3) Fikiria mabadiliko ya geografia, utamadum na makaribisho. Panga makanisa yaliyo karibu zaidi na mahali panapolengwa kigeografia na usimamishe kanisa mahali hapo kitamaduni.

4) Jibu maswali yafuatayo kulingana na hali inayoonekana katika ramani na maelezo yaliyopeanwa hapo chini ya ramani.

   a) Ungesimamisha kanisa la kwanza wapi (kila hrunifi inawakilisha mahali panapohitaji kanisa)?

   b) Ni katika sehemu gani ungetuma wafanya kazi walifunzwa katika kanisa la msingi?

   c) Ungewezaje kupanga kufikia sehemu zote?

Gografia utamaduni na makaribisho



e. Kundi lifanye agano pamoja. Lazima wajitoe kwa Mungu na mmoja kwa mwingine kwa heshima ya kufikia makanisa.

f. Omba na kufunga (Matendo 13:1-3).

g. Watie wengine waliombee kundi (2 Thes 3:1).

Mahali Pa Majadiliano

Jambo la kutenda lililoelezwa hapo juu linahusianaje na utamaduni na mazingira yako?

B. Jambo la kutenda #2: Panga Kundi Lako.

1. Utangulizi wa kupanga kundi lako.

   a. Mfano wa Agano jipya ni kusimamisha makanisa katika makundi.

      1) Petro alikwenda na wengine kufanya uinjilisti katika kaisaria (Matendo 10:23).

      2) Paulo and Barnabas (pia Marko, Luka, na wengine) waliunda kikundi (Matendo 13:2).

   b. Katika jambo hili tutafanya hivi:

      1) Unda kikundi.

      2) Kutana pamoja kupanga.

2. Kunda kikundi.

   a. Omba kwa ajili ya kusimamisha kundi. Yesu aliomba usiku kucha kabla hajachagua kundi lake (Lk 6:12, 13).

   b. lmarisheni mpanga kuhakikisha kwamba kuna kazi ya kujitolea yenye nguvu.

      1) Njia nzuri ya kufanya hili ni kuendeleza kujitowale kwa nguvu kwa Yesu na kwa washirika wale wengine wa kundi.

      2) Hili linatimilizwa kwa kunda uhusiano wenye nguvu.

Maelezo Mafupi –

3. Kupanga.

   a. Maswali ya kuuliza katika mikutano.

      1) Nani atawajibika na kundi? Kuwajibika huku kutatiwaje katika mazoea?

      2) Kundi litahitaji pesa gani? Kundi litazipataje?

      3) Uongozi wa Kanisa lililosimamishwa utaundwaje?

   b. Mambo ya kufanya mikutanoni.

      1) Omba.

      2) Kata kauli juu ya masomo na yafanywe upya pamoja na mipango ya kusimamisha kanisa litakalotumiwa.

      3) Jifunze ni ramani mnapojadili mpango.

      4) Tafuteni njia za kupata maandiko katika lugha ya kundi linalolengwa .

      5) Jadilini yote yanayohusu maisha ya kawaida ya kundi (nyumba, chakula, wakati wa jamaa, nyakati za kazi).

      6) Fikiria vipawa vya kila mshirika wa kundi, gawanya madaraka kulingana na vipawa hivi.

      7) Mkutano wa mwisho uwe wa kupeana huduma kwa kundi (Matendo 13:1-3; 15:40).

         a) Ripoti yaweza kupeanwa katika mwili mkubwa wa Kristo ambao unapeana mazaada kwa umishonari.

         b) Washirika wa Kundi wanaweza kuimarisha tena kujitolea kwao kwa umishonari na mmoja na mwingine.

         c) Kanisa linalotuma laweza kuliombea na kuwekelea mikono kundi.

Mahali Pa Majadiliano

Jambo la kutenda lilioelezwa hapo juu linahusia naje na utamaduni na mazingira yako?

C. Jambo la kufanya #3: Zoeleana Na Watu.

Maelezo Mafupi -

1. Utangulizi kwa kuzoeleana na watu.

   a. Paulo alihusiana na watu kwa makini na mazingira ya waatheni. Kisha akawazungumiza watu kwa njia iliyohusiana nao. (tazama Matendo 17:16-34).

   b. Katika jambo hili la kutenda tutafanya haya:

      1) Tutakata kauli ni namitutawapatia injili kwanza.

      2) Tutazoeleana na watu.

2. Ninani tutawapa injili kwanza?

   a. Makanisa wengine hukua vizuri yanapoundwa kulinga na kundi lile lile la kitamaduni (hii inaitwa "Sehemu zinazofanana kwa maumbile" kanuni ya kukua kwa kanisa). Lenga moja ya kundi la watu lililoelezwa vizuri.

   b. Kwanza, tumia "uunganishaji" wowote ambao ungeweza kupata. Tembelea jamaa au rafiki wa wale walio katika kundi an katika Kanisa linalotuma.

   c. Fanya uinjilisti katika hali za asili mwanzoni. Tembelea majirani. sema na watu sokoni mahali pa mafunziko uwanjani na katika basi.

   d. Shiriki katika mambo ya kutenda ya jamii. Anza mazungumzo na watu ambao yanaweza kuongoza kushuhudia. lnjili huenca kiasili kwa uhusiano wa kazi zote. Hata yaweza kuwa inawezekana na kuwa ya faida kujiunga na mashirika.

   e. Viongozi wa jamii ni kina nani? Ni watu gani wanaowavutia wengine kuna faida ya muhimu kuwapa injili viongozi kwanza. Wanaweza kutoa misingi wa asili wa uongozi kanisani.

   f. Kwa kawaida, uwe mwangalliaji na mwana funzi.

   g. Kama likifanywa kwa kujilisi, maswali yanawe za kutumiwa kungamisha na kujifunza juu ya watu washirika wa kundi waweza kwenda nyumba kwa nyumba.

Maelezo Mafupi –

3. Kufahamiana na watu.

   a. Ni muhimu sana kuwajua watu. Utakuwa mwinyilisti mzuru ukijua imani na mahitaji ya watu.

   b. Maswali yafuatayo yange fikiriwa. Tumia werevu kupata maelezo ya lazima.

      1) Dini yao ni gani?

      2) Wana mazoea ya desturi gani za dini?

      3) Mbona wanazizoea?

      4) Wanaamini nini juu ya Mungu?

      5) Wanamwa buduje?

      6) Wanajua na kuamini nini juu ya Yesu?

      7) Wanaamini nini juu ya mbinguni na kuzimu?

      8) Wanaamini nini juu ya Uumbaji?

      9) Wanaamini nini juu ya Uumbaji?

      10) Wanaamini nini juu ya pepo wachafu?

      11) Wanaamini kunatendeka nini kwao baada ya kifo.

      12) Wanaamini nini juu ya dhambi na wokovu.

      13) Wanajua nini juu ya Kanisa? Ni kukubali?

      14) Wanaamini nini juu ya maombi?

      15) Ni shida na mahitaji gani yaliyo ya kawaida sana kwa watu?

      16) Wanafanya kazi za aina gani?

      17) Kiwango chao cha uchumi ni gani?

Mahali Pa Majadiliano

Maelezo Mafupi -

Mambo ya kufanya yaliyofafanuliwa hapo juu yanahusianaje na utamaduni na mazingira yako?

D. Jambo la kufanya #4: ltisha Ushindi Wa Kristo.

1. Utangulizi wa kuuliza ushindi wa Kristo.

   a. Chukua muda kujifunza Maandiko yafuatayo pamoja na kundi lako.

      1) Biblia husema juu ushindi mwingi uliofuata maombi na kufunga.

      2) jifunze na ujadili Waefeso Eph 6:10-20. Lenga hasa juu ya vifungu. 12, 13.

      3) Fikiria jufunze na jadili 2 Kor 4:4; Uf 12:11; Wakolosai 2:15; Waebrania 2:14,15; Rum 1:4; 2 Kor 10:3, 4; na Dan 9:1-3.

   b. Tendo hili lazima lifanywe katika mwenendo wote wa kusimamisha makanisa. Hata hivyo, hapa twataka kulenga juu ya vita vya nguvu vya kiroho katika kufitayarisha kwa uinjilisti zaidi wa nguvu.

2. Panga na uwe na nyakati za nguvu za maombi na kufunga.

   a. Omba kwa ajili ya kupambanua roho. Ni nguvu gani muhimu za kiroho ambazo zinahitaji kuharibiwa katika sehemu hiyo?

   b. Omba nguvu za Mungu zidhilishwe.

   c. Ombea roho ziokolewe.

   d. Tangaza mamlaka na ushindi wa Yesu Kristo juu ya nguvu za kiroho za eneo hilo.

   e. Endelea kuomba mpaka usikie kwamba umepata ushindi.

Maelezo Mafupi –

Mahali Pa Majadiliano

Jambo la kufanya lililoelezwa hapo juu linahusianaje na utamaduni na mazingira yako?

E. Jambo la kufanya #5: Tafuta watu wanaopokea.

1. Utangulizi kwa kutafuta watu wanaopokea.

   a. Katika sehemu hii inatupasa kuwaendea watu wengi kama iwezekanavyo (Yn 1:41, 42).

      1) Tulenge vichwa vya nyumba yote.

      2) Sisi tu kama wavuvi wanaotupa nyavu zao kwa upana ili wavue samaki kiasi kizidi. Halafu tunavuta wavu ndani na kuwavua wale ambao wanapendezwa sana (Mt 4:19; Matendo 17:34).

      3) Sisi tu kama wakulima wanaopanda mbegu katika aina zote za ardhi lakini wanaofikiria kwa makini juu ya udongo ambao una uwezo wa kuleta mavuno mengi (Mt 13:3-7,18-23).

      4) Usitumie wakati mwingi na wale ambao hawa pendezwi au na wale ambao wanaonyesha upinganizi mkubwa (Mt 7:6).

      5) Wape nafasi ya kwanza wale wanaopokea sana. Paulo, kwa mfano, alikwenda kwa mataifa kwa kuwa walikuwa wanapokea kuliko Maya hudi.

   b. Katika jambo hili la kutenda tutajaribu kuwaendea watu wanaoipokea injili.

2. Ombea "makarisho ya Mungu" Roho Mtakatifu aweza kuwaongoza kwa watu wonaopokea (tazama Mt 13:3-7, 18-23). weka lengo. Unataka kuwaendea watu wangapi? Ni wangapi utakaoendelea kuwaendea zaidi?

3. Fikiria na ukubali juu ya mifano ya kufaulu na kuleta matokeo mazuri katika uinjilisti. Utawaendeaje? Fanya mpango. Rudia maelezo uliyo nayo kutoka jambo la kufanya #3. Hili litakusaidia kukata kauli katika njia za werevu.

4. Tia mpango katika matendo. Fanya hivyo!

5. Kagua kazi yako.

   a. Ulifikia lengo lako?

   b. Ni mipango gani iliyofanya kazi?

   c. Ni mipango gani iliyobadilishwa?

   d. Watu walipokeaje njia uliyoitumia?

6. Tumia kanini za kuzidisha ili kuwaendea watu zaidi. Nenda na wale ambao wamekwisha kuonyesha upendeleo wa kuwatembelea jamaa zao na rafiki zao.

7. Tumia "injili kwa wote" (mahitaji ya huruma) kufanya kazi pamoja na "injili ya winjilisti" (mahitaji ya kiroho). ltikia mahitaji ya mwili na yanayogusika.

   a. Onyo: Usikubali huduma za jamii kudhoofisha kazi ya unijilisti Wapatie injili wale wanaokuja kwa misaada.

   b. Unapotafuta kuwavutia watu wapya, imarisha miraidi ambayo tu na huduma ambazo kanisa jipya linaweza kudumisha, hasa kama wakisema mahitaji yanayogusika.

Mahali Pa Majadiliano

Jambo la kutenda lillilofafanuliwa hapo juu linahusianaje na utamaduni na mazingira yako?

F. Jambo la kutenda #6: Fundisha injili.

1. Utangulizi kwa kufundisha injili.

   a. Mvuvi huvuta wavu ndani kwa wangalifu sana Hataki kupoteza samaki kwa sababu tu ya njia mbaya ya kuwavuta ndani.

   b. Ni vivyo hivyo kwa uinjilisti. Lazima tuhakikishe kwamba tunatoa injili wazi ili tusiwapoteze samaki kwa sababu tu ya njia usiyofaulu.

   c. Lazima tuilinde na tufundishe injili kwa wale wanaopendezwa (Matendo 19:8).

Maelezo Mafupi –

2. Omba hekima na uwazi katika vile unafundisha injili kwa walio na upendeleo unaowaendea.

3. Panga mradi.

   a. Utafundisha nani? Lenga kufundisha makundi badala ya watu binafsi (jamaa, makundi ya jirani au rafiki.).

   b. Nani atakayewafundisha?

   c. Utawafundisha lini na wapi?

   d. Utawafundisha nini? (tazama Lk 24:44-48)? Fikiria pia orodha ifuatayo.

      1) Mungu ni nani?

      2) Dhambi ni nini?

      3) Kifo ni nini?

      4) Hukumu ni nini?

      5) Yesu ni nani?

      6) Uzima wa milele ni nini?

      7) Kuzaliwa mara ya pili ni nini?

      8) Kipawa cha Roho mtakatifu ni nini?

      9) Kutubu na imani ni nini?

      10) Ubatizo ni nini?

      11) Kanisa ni nini?

   e. Mapendekezo ya mafundisho.

      1) Anza makundi ya nyumbani haraka iwezekanavyo.

      2) Jaribu kuhusisha mafunzo kwa yale wamekwisha kuyajua.

Maelezo Mafupi -

3) Tumia Biblia. Mpe kila mtu Biblia ikiwezekana. Tia moyo kila mmoja kusoma sehemu zinazoweza kutumiwa kwa matumizi maalumu kabla ya mkutano.

4) Kutaneni mara nyingi.

5) Eleza faida ya kumfuata Kristo. Eleza pia gharama.

6) Tia moyo jamaa na rafiki kufikiria kukata kauli pamoja.

7) Fahamu kuwako kwa mazoezi ya utumiaji wa nguvu za roho za angani katika maisha ya waongofu wapya.

   a) Mwongofu mpya lazima ajitambulishe, akiri, na kuacha mazoezi ya nguvu za roho za angani.

   b) Vitu vya dini ya nguvu za roho za angani lazima ziharibiwe.

   c) Nguvu za vyombo zivunjwe kwa maombi.

8) Saidia vichua vya nyumba kufunza jamaa zao.

9) Uwe na wakati wa kushirikiana na jamii na kufanya mambo ya mazoezi pamoja.

10) Fundisha juu ya ubatizo, Eleza kwamba ndiyo njia ambayo kwayo mtu aweza kukata kauli hadharani kwa Kristo.

11) Ombea wagonjwa. Tarajia Mungu kuponya.

Mahali Pa Majadiliano

Jambo la kufanya lililofafanuliwa hapo juu linahusianaje na utamaduni na mazingira yako?

Maelezo Mafupi –

G. Jambo la kufanya #7: Kadiria matokeo.

1. Utangulizi wa ku chungulia matokeo.

   a. Fanya kazi yako ukiwa na lengo fikirani. Lenga kupata matokeo (1 Kor 9:22). Uwe na upendo wa kujikadiria mwenyewe kila mara. Hivi ndivyo tunavyoweza kuanza kuwa na matokeo mazuri.

   b. Katika jambo hili la kutenda tutafanya hivi:

      1) Toa injili kwa rafiki na jamii ya watu wanaopokea zaidi.

      2) Kadiria kazi ambayo tumekwisha kuifanya.

2. Fikiria wale ambao wamepokea zaidi. Waulize kuandika orodha ya jamaa wote na rafiki zao.

   a. Fanya mpango wa wale watakaowatembelea watu walio katika orodha na uonyeshe ni lini na kwa njia gani.

   b. Muulize mtu aliyetengeneza orodha kwenda nawe na kushiriki kwa nini anapendelea juu ya yale utakayoyasema.

3. Kadiria kazi.

   a. Umelenga kundi maalumu la watu?

   b. Je, Kristo yuko katika ya mafundisho yako?

   c. Watu waliomo katika makundi ya nyumbani waweza kueleza sehemu za msingi za injili? Je, wanajua jinsi ya kuomba? Wamekarivu sehemu zo zote za maandiko?

   d. Umelenga kutia moyo waongofu wapya?

   e. Ungali unatoa injili mara kwa mara?

   f. Umeendeleza uhusiano baina ya watu? Je, pana msingi mwema wa kuanzisha kanisa?

   g. Je, pana ukosefu wa kawaida wa kupokea katika watu wa eneo hilo? Kama ni hivyo, yawezekana kuwa wakati wa kwenda eneo jingine (Mt 10:14).

h. Washirika wa kundi wanatimiza madaraka yao? Je, pana nidhamu katika kudumisha taratibu?

i. Je, washirika wa kundi wanatumia wakati wa kutosha pamoja na jamaa zao?

j. Je, pana hisi la nguvu la umoja baina ya kundi?

k. Pana mapingamizi baina ya washirika wa kundi ambayo yanahitaji kurekebishwa?

l. Tunahitaji kwenda wapi baada ya hapo? Je, tunahitaji kurudia mazoezi mengine ya hapo awali

Mahali P Majadiliano

Jambo la kutenda lili lofafanuliwa hapo juu linahusianaje na utamaduni na mazingira yako?

H. Jambo la kufanya #8: Wabatize na uwapokee washirika katika Kanisa jipya.

1. Utangulizi wa kupokea washirika wapya.

   a. Fahamu kwamba ubatizo ni sehemu ya muhimu ya kutumwa au mwito mkuu (Mt 28:19).

   b. Fahamu pia kwamba katika Biblia ubatizo haukucheleweshwa (Matendo 16:31-33).

      1) Katika Agano Jipya watu hawakuinua mikono au kuja madhabahumi penye kiti cha rehema walibatizwa!

      2) Ubatizo haukuwa kipawa ausherehe ya kutenuliwa amabayo ilifanywa baada ya darasa refu la ushirika wa kanisa. Ulikuwa unafanywa wakati wa kuokoka na ukawakilisha mwanzo wa maisha ya ukristo.

   c. Katika jambo hili la kufanya tutafanya hivi:

      1) Tuwabatize waongofu wapya na tuwapokee kama washirika wa Kanisa jipya.

      2) Tusherehekee chakula cha Bwana kama Kanisa jipya.

Maelezo Mafupi –

2. Hapa, fanya mafunzo ya ubatizo rahisi (tazama Mt 28:19, 20; Matendo 8:35-38; 10:47, 48; 2:41-47; 16:31-33).

   a. Kaza kwamba ubatizo ni njia ya biblia kutangaza hadharani imani katika kristo na kujitambulisha na Kanisa Lake.

   b. Wabatize jamii wote pamoja ikiwezekana (Matendo 16:15, 31-33).

3. Mapendekezo kwa ibada ya ubatizo.

   a. Mkubali mwongofu kutoa ushuhuda wake, kisha umbatize.

   b. Mwekelee mikono na uombe kwamba ajazwe na Roho mtakatifu (Matendo 8:17).

   c. Sherehekeeni Meza ya Bwana pamoja.

4. Mapendekezo kwa sherehe ya Meza ya Bwana.

   a. Jaribu kufanya hali kuwa ya asili. Kusanyikeni kuzunguka meza ikiwezekana.

   b. Chukueni wakati wa kuimba nyimbo za sifa nyingine.

   c. Chukueni wakati wa kuomba. Uliza kila mtu aombe kwa unyamavu na wakiri dhambi zao. wahakikishie msamaha wa Kristo.

   d. Mahali hapa usijaribu kueleza madhehebu juu ya chakula cha Jioni. Hakikisha kuonyesha hali ya kumcha Bwana.

5. lfanye kuwa wazi kwa kundi jipya la waongofu kwamba wao sasa ni kanisa.

   a. Rudia mafunzo ya misingi kuhusu maelezo na maisha ya Kanisa.

   b. Anza kuendeleza maono ya kuwa na viongozi wa mtaa.

   c. lmarisha njia amabayo washirika wapya wanaweza kufanya agano mmoja kwa mwingine.

Mahali Pa Majadiliano

Jambo la kufanya lililotajwa hapo juu linahusianaje na utamaduni na mazingira yako?

KUSIMAMISHA KANISA

Maelezo Mafupi -

I. Jambo la kufanya #9: Wafunze wote kutii Kristo.

1. Utangulizi wa kufundisha wote kumtii kristo.

   a. Sehemu ya kazi yetu kama wasimamishaji wa Kanisa ni kuwafundisha watu kutii sheria za Kristo (Mt 28:20).

      1) Lazima tuwazae wanafunzi wanaopendelea kutii sheria za Kristo. Kwa kweli hakuna aina nyingine za wanafunzi.

      2) Ni kawaida kwa Mkristo kutaka kutii amri za Kristo. Bila utiifu kuna imani iliyokufa (Yakobo 2:14-17).

      3) Hatuokolewi na matendo (Waefeso 2). Lakini tunaokolewa kufanya kazi nzuri (Yakobo 2)

   b. Katika jambo hili la kufanya tutawafundisha waamini wapya kutii amri za Kristo.

2. Orodha ifuatayo ya amri za muhimu lazima ifundishwe katika mkutano ya kwanza ya kanisa.

   a. Tubu na uamuni (Mk 1:15; Yohana 3:16).

   b. Ubatizwe (Mk 16:16; Matendo 2:38).

   c. Mpende Mungu, jirani yako, na ndugu zako katika Kristo (Mt 22:37-39; Yn 13:34).

   d. Kutaneni kushirikiana chakula cha Bwana (Lk 22:17-20).

   e. Omba na usome Biblia kila siku (Mt 4:4; 6:5-13; Yn 14:15).

   f. Peana kwa kujitolea (Mt 6:19-21).

   g. Hubiri injili na uwafundisha wengine (Mt 28:18-20; Mk 16:15).

3. Andika orodha ya waongofu wapya. Andika kila awu juu ya kila karatasi. Andika maelezo ya vile kila mmoja anaendelea katika kutii kila anui.

   a. Je, waongofu wapya wanawapa walio na mahitaji? Wanashirikiana na kuwa mawakili wema?

   b. Wanaimarisha ao ya maombi ya kila siku?

4. Fanya ushirika kuwa jambo la mulimu katika kanisa jipya. Panga nyakati za kujibuudisha na kula pamoja.

5. Funza juu ya fungu la kumi na upokee sadaka. Mwe na mkutano ya maombi na mkate kauli vile pesa zitatumika.

Mahali Pa Majadiliano

Jambo la kufanya lilioelezwa hapo juu linahusianaje na utamaduni wako na mazingira?

J. Jambo la kufanya #10: Mwe na mikutano ya kuabudu.

1. Utangulizi wa kuwa na mikutano ya kuabudu.

   a. Waongofu wapya lazima wajue kwamba wao ndio kanisa jipya (si kundi) na lazima wakutane pamoja (Waebrania10:25).

      1) Kanisa jipya liwe na kitambulisho chake lenyewe mikutano isifanywe tu kama vile washirika wa kundi wamezoea. Kundi liwe na mindo wa maneno ya kuabudu.

      2) Usiongoze mikutano kwa njia ambayo waongofu wapya wataona shida kuiga.

      3) Fanya mikutano kuwa rahisi na ya asili.

   b. Katika jambo hili la uifanya tutafanya haya: Anza kuwa na mikutano ya kuabudu katika mtindo rahaisi ambao unaweza kuigwa kwa urahisi na viongozi wa mtaa walio na uwezo wa kukua wakati ujao.

Maelezo Mafupi –

2. Fikiria njia ambazo kwaza waweza kuendeleza mtindo ufaao wa kuabudu.

   a. Kumbuka: Hili si kanisa la Kundi. Ni kanisa la waamini wapya. Watataka kuabudu kulingana na utamaduni wao wenyewe.

   b. Fikiria maswali yafuatayo.

      1) Wanacheza vifaa gani vya muziki?

      2) Tungeweza kutumia muziki wa watu kuunda nyumbo mpya za kuabudu?

      3) Je, washirika wote wanawezaje kushiriki katika ibada ya kuabudu?

      4) Ni njia gani inayoweza kuwa nzuri zaidi ya kufundisha?

         a) Mafunzo mafupi ya Biblia?

         b) Mahubiri ya kawaida?

         c) Michezo ya kuigiza ya hadithi za Biblia?

      5) Ni aina gani ya maombi ingeweza kukubaliana zaidi na utamaduni?

         a) Unyamavu?

         b) Maombi ya Makundi?

         c) Kupiga magoti?

         d) Kusimama?

         e) Kuketi?

         f) Mikono ikiinuliwa?

      6) Mngekutana wapi? Wakati gani?

         a) Kuna faida (asa mwanzoni) ya kukutana nyumbani.

            (1) Faida inayoonekana wazi ya fedha.

            (2) Kuna zaidi ya hali ya hewa ya kawaida ambayo inaweza kuleta uhusiano wenye nguvu.

(3) Kuna mengi ya kuimarisha zaidi kwa huduma ya mazoezi.

(4) Kumbuka: kanisa la Agano jipya lilikutana nyumbani.

b) Kuna faida ya kukutana katika majengo ya makanisa.

(1) Kwa kawaida mna nafasi kubwa .

(2) Hauwi mzigo kwa jamaa moja.

(3) Kuna makatizo machache tu.

c) Mahali pa mkutano pawe:

(1) Karibu na nyumba za watu.

(2) Panaweza kupatikana panapohitajika.

(3) Panaweza kulipika (kama kuna malipo ya nyumba, reheni, n.k).

(4) Panaburudisha ya kutosha kwamba watu wanajisikia huru kuabudu.

(5) Pakubwa kutosha kutoshea kila mtu.

(6) Pa kudumu haraka iwezekanavyo.

d) wakati wa mkutano uimarishwe juu ya:

(1) Nyakati za kazi na za mlo.

(2) Desturi.

(3) Taarifa ya usafisrishaji wa watu wote.

(4) Siku za soko.

c. Jaribu kuongoza ibada ya asili (tazama 1 Kor 14:26).

1) lwe na kuhisi mpango pamoja na kuhisi kujitolea, wahausishe washirika wa kanisa. Waonyeshe kwamba ni kanisa lao. Endeleza uwezo wa viongozi wa asili.
2) Mapendekezo ya ibada katika kanisa jipya.

Maelezo Mafupi

a) Uwe na mwanzo na mwisho ulio wazi.

b) Weka lengo juu ya Yesu.

c) Panga njia ya kuhusisha washirika wote.

d) Endeleza hali ya hewa ambapo watu wanasikia huru kukiri dhambi mmoja kwa mwingine (Yakobo 5:16).

e) Tia mkazo kupatikana kwa msamaha wa Mungu.

f) Fanya meza ya Bwana katikati mwa kila ibada.

g) Ombea wagonjwa.

h) Peana mafunzo mafupi ya rahisi.

i) Patia watu wote nafasi kujibu ujumbe kwa njia fulani.

j) Endeleza ushirika kabla na baada ya ibada. Uwe mwanzilishi katika vile utalifanya.

k) Chukua sadaka katika njia inayofaa ya kitamadum.

l) Panga jambo la muhimu kwa watoto.

m) Kubali washirika wengine wenye vipawa wahudumie kwa muziki maalumu.

d. lbada ya kuabudu isifunguliwe kwa "umati" (lbada ifanywe kama kundi ndogo la pekee) mpaka viongozi wa mtaa waweze kuongoza ibada.

Mahali Pa Majadiliano

Jambo la kufanya lililoelezwa hapo juu linahusianaje na utamaduni na mazingira yako?

K. Jambo la kufanya #11: watayarishe Waongofu wapya.

1. Utangulizi.

   a. Wakristo wote wawe mashahidi wa Kristo kanisa jipya litakua wakati waamini wapya wataanza kushududia.

      1) Lazima wajifunze kushuhudia.

      2) Lazima wataya rishwe na wafundishwe (tazama Mt 4:19).

   b. Katika jambo hili la kufanya tutawasaidia waongofu wapya kuhubiri injili.

2. Anza kulenga mafundisho yako juu ya kuhubiri injili. Eleza kusudi na umuhimu wa kuhubiri injili na umishonari.

   a. Uliza kila mwongofu mpya kufanya orodha kamili ya rafiki zao na jamaa. Hao walio katika orodha wanaoishi katika sehemu nyingine waweza kuendewa kwa kusimamisha makanisa mengine mapya.

   b. Waeleze kuomba juu ya orodha kila siku.

      1) Omba kwa imani. Mungu aweza kuokoa mwenye dhambi aliye mbaya zaidi.

      2) Omba kwamba Mungu angetayarisha mioyo yao kupokea neno la Mungu na waokolewe.

3. Wakati wo wote mshirika wa kundi aendapo nje kuhubiri injili alete mwongofu mpya. Waende kwa watu katika orodha ya waongofu.

   a. Mshirika wa kundi aongoze majadiliano mpaka mwongofu mpya amepata imani ya kutosha kuongoza.

   b. Tia moyo mwongofu mpya kuwa mwenye kuanzisha vile atatoa injili. Mweleze kwamba aweza kutumia njia zake anazozifiria kuwa za kufaulu. Hata hivyo, kaza umuhimu wa neno la Mungu, na asili yake ya kuokoa

   c. Watie moyo waongofu wapya kwenda sehemu nyingine na kusimamisha makanisa. Usingoje lzidisha maono ya kusimamisha maikanisa haraka iwezekanavyo.

Maelezo Mafupi –

4. Mahali hapa, washirika wa kundi la kusimamisha makanisa wawapatie SILAHA waongofu wapya. lnawapasa kuwafundisha jinsi ya kufundisha, kutoa injili, kupanga kuongoza mikutano, kuwobatiza wengine, n.k.

   a. Uongozi wa mtaa wanze kuundwa.

   b. Kufanya hivi ni ya muhimu sana kulenga kuuliza mashauri ya viongozi wanaokua. Lazima watiwe kazini na mapendekezo yao lazima yafuatwe.

      1) Kwa njia hii watahusishwa.

      2) Watajifunza pia umuhimu wa kufanya kazi katika kundi.

Mahali Pa Majadiliano

Jambo la Kutenda lililofafanuliwa hapo juu limehusianaje na utamaduni na mazingira yako?

L. Jambo la kufanya #12: Kuwafunza viongozi.

1. Utangulizi kuwafunza viongozi.

   a. lli kuzidisha kuje lazima pawea na kuendelea kuzaana kuliko wazi. Viongozi lazima wajitambulishe na wawafunze viongozi (Tito 1:5).

   b. Katika jambo hili la kufanya tutawunda uongozi wa Kanisa jipya.

2. Viongozi wa mtaa lazima wafunzwe kusaidia washirika wa kanisa kukua, kukuza huduma kadha, na kusimamisha makanisa.

   a. Omba na ufunge juu ya mambo ambayo angefunzwa kama kiongozi (tazama Matendo 14:23; tumia 1 Tim 3:1-7 na Tito 1:5-9 kama ya kuongoza).

   b. Chagua vifaa vya kufundisha kutumia kosi katika MOTMOT).

   c. Anza na misingi na ulenge jinsi ya kufanya jambo.

      1) Uinjilisti.

      2) Uanafunzi.

      3) Maombi.

4) Kanuni za uongozi.

5) Ubatizo.

6) Kusifu na kuabudu.

3. Fanya mpango halisi wa ni lini na jinsi gani utaondoka.

a. Ni tarehe gani utaweza "kuwapatia Bwana" (Matendo 14:23).

1) Uwe na hakika kwamba pana kundi la kuaminiwa na viongozi walio na uwezo.

2) Usingoje muda mrefu kuondoka. Usingoje mpaka viongozi wapya na kanisa jipya "waimarike" ukubali kuchukua jambo la kujihatarisha.

b. Kundi litakwenda wapi sasa? Watadumishaje kuliiendea kanisa jipya? Kundi litabaki lilivyo?

Mahali Pa Majadiliano

Jambo la kufanya lililofafanuliwa hapo juu huhu sianaje na utamaduni wako na mazingira?

Kusimamisha Makanisa: Maneno Ya Mwishoni

Maelezo Mafupi -

[1]George Patterson, Uongozi Wa Kusimamisha Makanisa. Grand Rapids: Baker Book House, 1989. Mtiririko wa mambo makubwa ya muhtasari wa sehemu hii ya kosi umechukuliwa moja kwa kutoka katika mafunzo ya George Patterson. Imetumiwa kwa kuhusiwa.

[2]Larry Tomczak, "Kufahamu Huduma ya kusimamisha Makanisa" (Gaithersburg, MD: People of Destiny International, 1987). Mawazo mengine ya kosi hii katika kwaisa za kwanza nne zimenakiliwa kutoka katika Tomczak .

[3]Glen J. Yoder, Maanidko ya darasa katika kosi iitwayo "kanuni za kukua kwa makanisa"", Regent University, 1987. "Hatua sita za kusimamisha makanisa" na mchoro unafanana zilinakiliwa kutoka mafunzo ya Yoder.

KUSIMAMISHA KANISA

Maelezo Mafupi -